Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba

## Utangulizi

Hujambo na karibu tena katika kipindi cha sikiliza ujifunze juu ya afya. Umewadia tena wakati wa kujiunga na Manuel, Simo, Jimmy, Steve na Hassan katika bweni la Mandela tusikie leo wana yapi? Kumbuka vijana hawa wamekuja mjini kujiunga na shule ya upili kwa kuwa kijijini kwao hakuna shule za upili. Je nini kitatokeo leo hii? Naam kwa kweli pilka pilka sio nyingi kwa sababu Jimmy ni anaugua kama mbwa. Tusikie nini kimemsibu… Hali kadhalika tutakufahamisha kuhusu jinsi unavyoweza kuwaepuka kunguni… kwa sababu hao ndio tatizo kubwa linalowakera rafiki zetu… Tega sikio…

## Tukio la kwanza

*Muziki. Wahusika, Hassan na Jimmy ndani ya mweni asubuhi.*

*SFX* *Chooni mvumo wa wadudu kama nzi..sauti ya redio ya Hassan inasikika kwa mbali,,,,muziki wa Usher Raymond…*

Hassan: (Kando ya Mic) Oh Jimmy unaonekana kama mtu anayekufa… una nini? Funga dirisha… harufu yote ya chooni inaingia ndani…

Jimmy: (Kwenye Mic) Samahani mshikaji… naumwa na tumbo ile mbaya…

Hassan: (Kando ya Mic) Unaharisha?

Jimmy: (Kwenye mic) Yaani ni mchanganyiko wa mvurugiko wa tumbo, (alalama kwa uchungu) naona ntapiga kambi hapa chooni… Lo…

Hassan: (Kando ya Mic) Lo… Jimmy umeingia chooni kama mara sita hivi katika muda wa saa tatu siutaishiwa pumzi humo ndani kwenye choo hicho kinanuka kama nini…

Jimmy: (Kwenye Mic) (kwa uchungu) Naumwa kweli Hassan… wacha nitoke nije nilale kifudifudi kitandani, siwezi hata kusimama wima.

Hassan: (Kando ya Mic) Nenda hospitali wewe…

Jimmy: (Kwenye Mic) Sina pesa… auchiii… kwanza naingia chooni…

*SFX* *Mlango wa mabati unafunguliwa na kufungwa kwa kutumia nguvu*

Jimmy: (Kwenye Mic) Mlango huu… naufunga kwa nguvu… (ajitahidi kupambana na mlango huku ana maumivu)

*SFX* *Mlango unaanguka Jimmy anakoroma kwa maumivu*

Hassan: (Kando ya Mic, anacheka) Nilisema mimi siku moja mlango huu utakuja kuleta aibu… sasa fikiria ingekuwa umeanguka baada ushavua suruali ingekuaje…

Jimmy: (Kando ya Mic) Mlango huu, umenikata bwana…

Hassan: (anapiga kelele kutoka mbali) Jimmy kuna nini?

Jimmy: (Kando ya Mic, akiwa na maumivu) Huu mlango wa kipuuzi umenikata mkononi…

Hassan: Njoo hapa tukuoshe na chumvi…

Jimmy: (Anakaribia) Lo! Ni siku gani hii… kila kitu nuksi…

Hassan: Nafikiri afadhali uende hospitali…

Jimmy: (Kwenye Mic) Utanikopesha pesa? Steve hajanilipa bado.

Hassan: Lo, utanisamehe sana mshikaji wangu… nimebakia na pesa kidogo tu za kutumia kama nauli ya kurudi nyumbani tukifunga shule. Na nikishindwa kurudi nyumbani, inamaanisha ntashindwa kuchukua karo ya muhula ujao kutoka nyumbani.

Jimmy: Ni sawa Hassan wewe nipe ntakuwa nimeshakurudishia ukifikia wakati huo.

Hassan: Ok Jimmy chukua hizi basi wewe nenda kamuone Dokta au vipi… Poa.

**Tukio la pili**

*Nesi mwanamme na Jimmy katika kliniki nyakati za asubuhi inakaribia mchana*

*SFX:* *Hakuna shughuli nyingi,sauti za watoto wakilia,watu wakikohoa, wakipiga chafya, na mazungumzo ya kila aina mlango unafunguka na sauti ya mwanamme inasika ikiita majina.*

Nesi: Mwengine…

*SFX* *Sauti ya miguu ikitembea halafu anavuta kiti kukaa.*

Nesi: Jina lako? Umekuja kwa sababu ya hicho kidonda hapo… au tukusaidieje?

Jimmy: Naitwa Jimmy,,,na niko hapa kutokana na matatizo kadhaa ya mwilini.

Nesi: Matatizo kama yapi?

Jimmy: Naharisha sanaa

Nesi: Kwa muda gani umekuwa na matatizo haya?

Jimmy: Hii ni siku ya tatu…

Nesi: Umetumia dawa zozote hapo kabla?

Jimmy: Hapana, nilikuwa nikilala tu kwenye bweni, sikuwa na pesa za kuja kwa matibabu mpaka rafiki yangu aliponikopesha hii leo.

Nesi: Unapaswa kuwa makini na maradhi yote kwa sababu ukiwa sio muangalifu unaweza kupoteza maisha yako. Kuharisha

kwa siku mbili bila ya kupata matibabu ni hatari sana unaweza kupoteza maji mwilini.

Jimmy: Kwa kweli  najihisi vibaya kweli hivi sasa. Naweza kuingia chooni kwanza?

Nesi: Sawa unaweza kujisaidia… Choo kile.

Jimmy: Ooooh afadhali sasa limetulia kidogo… tunaweza kuendelea sasa nesi…

Nesi: Sawa… Umekuwa ukila chakula gani siku mbili zilizopita?

Jimmy: Maharagwe na viazi…

Nesi: Hivyo sio vyakula vya mafuta mengi?

Jimmy: Hapana nilikuwa nikitamani sana vyakula hivyo na mamangu kila mara alikuwa ananiambia nile vyakula vyote ninavyovipenda wakati nikiwa mgonjwa. Na nilikuwa sina vyakula vingine vya kuchagua… na ni suala la pesa pia… Maisha mjini ni ghali sana kwangu mimi na rafiki zangu.

Nesi: Ok… Mnapika wenyewe chakula au mnakula hotelini…?

Jimmy: Kusema kweli tunajipikia wenyewe…

Nesi: Mnakula chakula cha moto?

Jimmy: Siku ya kwanza ndio tunakula kikiwa moto. Lakini kwa sababu tunabania matumizi, tunaangalia tusiishiwe na mafuta ya jiko tunapika chakula kingi mara moja halafu tunakipasha moto tu kila siku mpaka kitakapokwisha.

Nesi: Sawa! Mnakihifadhi vipi chakula chenu? Mna oven au jokofu la kuweka chakula cha kubakia?

Jimmy: (Acheka) Nesi usinichekeshe… tutawezaje kumudu kununua jokofu wakati umeme tulikatiwa na mwenye nyumba kwa kukosa kumlipa.

Nesi: Sasa mnakihifadhi vipi chakula chenu? Mnakifunika? Kuna panya mnakoishi na mende, na wanyama wengine wadogowadogo?

Jimmy: Hapana… tunakiweka chini ya mvungu wa kitanda… na… ndio… kuna panya kibao na mende… panya buku lakini sio wengi nafikiri…

Nesi: Sawa… Nasikitika huenda ukawa umekula chakula kilichoharibika Jimmy.

Jimmy: Lakini kila siku tunajaribu kukipasha moto kabla hatujakula…

Nesi: Hiyo haitoshi… nzi panya na mende wanabeba viini vya magonjwa… Sasa binadamu akipata viini hivyo vinavvyoambukizwa na wanyama hao anaweza kupata maradhi mabaya na kufa.

Jimmmy: Sasa hiyo inamaanisha… ntakufa?

Nesi: Huwezi kufa… ntahitajika kukupima choo chako kikubwa?

Jimmy: Sawa Nesi…

Nesi: Baada ya uchunguzi… ntakupa dawa lakini lazima mujaribu kuwaangamiza panya na wanyama wengine wote wadogo wadogo huko nyumbani kwenu kwa kuyaweka mazingira kuwa safi.

Jimmy: Tatizo ni wenzangu tunaoishi pamoja… hawataki kufanya usafi…

Nesi: Ok Jimmy haijalishi marafiki zako wanachokifanya au kukisema…ni lazima usikize kwa makini na ufanye ninavyokwambia. Unatakiwa sio tu uwaangamiza panya lakini wanyama wote wanaobeba viini kama mende, kunguni, chawa na wengineo… Tunaelewana nnachokisema? Ni muhimu sana.

Jimmy: Lakini tutawauwa vipi nesi? Sasa hivi sina hata nguvu za kufanya lolote?

Nesi: Waambie rafiki zako wasafishe nje ya bweni lenu na ndani, fueni matandiko yenu yote… na hata kama huna nguvu… lazima uoge kila siku… (anacheka) najua suala hili ni gumu sana kwenu wavulana lakini usifanye maskhara na jambo hili…

Jimmy: Inachosha…

Nesi: Jimmy sikiza… lazima utie juhudi ukiwa unataka kuwa na afya tena na zaidi ubakie kuwa na afya! Ukiendelea kuishi na wanyama hao ndani ya bweni utakuwa mgonjwa kila siku… na usisahau unatakiwa unywe vitu vya majimaji kwa wingi… kama maji ya matunda, maji safi, supu na vinginevyo… ili urudishe nguvu… na pia ntakupa dawa za kutibu hicho kidonda chako lakini pia lazima ukiweke katika hali ya usafi.

Jimmy: Dakika moja nesi… lo nafaa… (avuta kiti na kukimbia, ajaribu kufungua mlango)… Chooo kiko wapi.

Nesi: Oh kijana huko sio chooni ni store ya dawa choo kiko upande wako wa kushoto…

**Tukio la tatu**

*Hassan, Jimmy, Manuel na Steve kwenye bweni saa tano asubuhi*

*SFX Mvumo wa wadudu kama nzi… radio inasikika kwa mbali na sauti za ndege…*

Hassan: Jimmy ilikuaje?

Jimmy: Ni wale panya…

Manuel: Niliwaambia jamaa… tutakufa hivi karibuni kwa sababu ya uchafu…

Hassan: Manuel muache Jimmy atuambie anachotaka kutuambia bwana…

Jimmy: Kwa kweli Manuel yuko sawa kwa kile anachotuambia kila siku… Kimsingi tunahitajika kuyabadilisha mazingira yetu kuanzia miili yetu hadi tunakoishi na nje.

Steve: Ni hayo tu kwa sababu ya panya? … Jamaa acheni mchezo… Soksi za Manuel zenye kunuka zitafanya hiyo kazi ya kuua panya.

Manuel: Sio tu kuhusu panya wewe Steve… kila siku nawaambia ni kuhusu kubadilisha mtindo wa maisha yetu… tunaishi vibaya sana jamaa.

Steve: Hubiri Manuel… ushafunguliwa uwanja… kwa jina la Jimmy na afya yetu tutawaangamiza wadudu waharibifu.

Jimmy, Hassan, na Steve: (wacheka na kuitika) Amen

*Muziki*

Je wajua kuhusu wanyama au wadudu waharibifu wa binadamu? Hawa ni wanyama au wadudu wa aina mbali mbali na hasa wale wanaohusishwa na maambukizi ya maradhi. Kwa ujumla hali ya hewa ya joto na unyevunyevu katika bara la Afrika inasababisha wadudu au wanyama wa aina hii kustawi. Wadudu au wanyama aina hii wanaambukiza binadamu maradhi mbali mbali ambayo ni hatari na yanaweza kusababisha kifo ikiwa hayatashughulikiwa.

**Wadudu au wanyama wenyewe**

Wale wadudu au wanyama wadogo kabisa walio katika kundi hilo ni pamoja na minyoo, amiba, na vijidudu vingine ambavyo haviwezi kuonekana kwa macho ya binadamu. Chawa, nzi na utitiri ni wakubwa lakini pia ni vigumu kuwagundua. Wadudu au wanyama wanaoweza kuonekana kama vile panya na panya buku wanaweza kuzuilika.

Maradhi yanayosababisha na wanyama au wadudu aina hiyo sio ukubwa unaojalisha hapa. Wadudu au wanyama wasioweza  kuonekana na macho ya binadamu wanaweza kusababisha matatizo makubwa. Wanaweza kusambaza magonjwa kama vile homa kali, homa ya vipindi, tauni, au kichaa cha mbwa. Maradhi yote haya ni hatari na yanaua ikiwa hayatatibiwa mapema. Minyoo midogo inaweza kuingia mwilini kutokana na uchafu. Ikiwa imeingia mwilini inashambulia viungo vya ndani kama vile ini, mapafu na utumbo. Dalili zake ni pamoja na kuumwa sana na tumbo na kupoteza damu. Maradhi yanayotokana na minyoo yanawakumba sana watoto. Na vile vile amiba inaweza kusababisha ini kushindwa kufanya kazi na hatiae kifo. Panya waweza kuambukiza maradhi kupitia mkojo, kinyesi na mate.

**Kinga**

Wadudu au wanyama wanaosababisha maradhi kwa binadamu wanakutikana zaidi katika vyombo vya nyumbani. Chawa au wadudu wakuruka wanaweza kuishi kwenye nguo chafu kama shuka au taulo. Hii ndio maana ni muhimu kufua nguo na matandiko ya kulalia mara kwa mara. Msivaliane nguo na matandiko bila ya kufua kwanza. Jiepushe kunywa maji ambayo hayajatibiwa na chakula ili kuzuia kupata minyoo. Matunda mabichi na mboga pamoja na nyama ambayo haijaiva vinaweza kuwa hatari kwasababu minyoo kwa kawaida inaweza kuishi

vizuri katika vyakula hivyo. Panya wanavutiwa sana na chakuala kilichooza na kwahivyo ni muhimu kutupa chakula aina hiyo mahala salama. Minyoo pia inaweza kukutikana kwenye ardhi na inaweza ikaingia mwilini ikiwa mtu anatembea miguu peku peku. Vaa viatu vya kufunika ikiwezekana. Pia kuna minyoo ambayo inaishi katika maziwa na mito… kwa hivyo jiepushe kuogelea katika maji ya kusimama. Mbwa na paka wanaweza kusambaza maradhi ya kichaa cha mbwa. Uking'atwa na mbwa au paka, hakikisha unaosha jeraha na sabuni na maji na umuone daktari haraka iwezekanavyo.